# WAKIZIONA NYAVU LAZIMA ZICHEKE

ISSNN 2347 - 4189 / Toleo Na. 0026 JUMATANO MACHI 5 , 2025 / Bei Tsh 1,000, Ksh. 100

SPORT MASTA






KUNA MTU ATALIA...

# YAGA SC WEBE, SIMBA SC UKUTA WA YERIKO

>> UK 2

## >> SASA SIKU ZINAANZA KUHESABIKA



# MUKWALA: KIKUBWA POINTI

## CHAMA KUMBE BADO WAMO

>> UK 2



# FADLU AITOLEA MACHO YANGA



>> UK 2

# YANGA WEMBE, SIMBA UKUTA WA YERIKO

NA MWANDISHI WETU

WAKATI zikiwa zimesalia siku nne pekee kuelekea mchezo wa ‘Dabi ya Kariakoo’ ambapo Yanga itakuwa mwenyeji wa Simba kwenye mchezo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumamosi wiki hii, kuna mambo kadhaa yamebainika kati ya timu hizo.

Yanga inaingia kwenye mchezo huu ikiwa timu iliyofunga mabao mengi zaidi kati ya timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ikifunga mabao 58 kwenye michezo 22 iliyocheza huku ikifungwa mabao tisa pekee.

Kwa upande wa Simba silaha yao muhimu mpaka sasa ni kuzuia mabao ambapo kwa msimu huu ndio timu iliyoruhusu mabao machache zaidi ikifungwa mabao nane pekee kwenye michezo 21 iliyocheza mpaka sasa huku ikifunga mabao 46.

Hii inamaanisha Yanga ina safu kali ya ushambuliaji ambayo haicheki na kima, kwani ukikaa vibaya tu lazima uchezee kichapo cha mabao mengi na kwenda kwenu kujiuliza.

Simba wao ni ‘Ukuta wa Yeriko’ hivyo, kutonekana kati ya safu mbili hatari zaidi, moja ikiwa wembe katika kufunga na nyingine ikiwa Madhubuti kwa kuzuia.

Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na alama 58 kwenye michezo 22 huku Simba ikiwa nafasi ya pili na alama 54 kwenye michezo 21 ikiwa na mchezo mmoja mkononi dhidi ya Dodoma Jiji utakaopangiwa tarehe mpya baada ya kuahirishwa kutokana na ajali iliyopata timu ya Dodoma mkoani Lindi.

# FADLU AITOLEA MACHO YANGA

NA ASHA SEKEFU

KOCHA wa Simba Fadlu Davids amesema mechi dhidi ya Yanga inaweza kutoa picha halisi ya ubingwa kwa timu yake msimu huu.

Fadlu amesema kama watapoteza mchezo huo, basi timu yake itakuwa imejiweka kwenye hatari kubwa ya kutwaa ubingwa, kwani itakuwa imepoteza pointi nyingi na itakuwa ngumu kumfikia aliyeko kileleni.

“Mechi kubwa zilizopo mbele yetu ni dhidi ya Yanga na ile ya Coastal ambayo tumeimaliza, hizi zingine tumeshamalizana nazo, lakini napata wakati mgumu kutokana na rekodi za mzunguko wa kwanza.

“Kwa sasa akili zipo katika mbio za ubingwa kwani bado ziko wazi na mwanga unaonekana ila tukifanya makosa mechi mbili zijazo nuru itazima kabisa.

“Hizi kwetu ni mechi inayobeba ajenda ya ubingwa na hatutacheka nayo kabisa, kwani tunahitaji alama tatu za nguvu zitakazotuweka katika nafasi nzuri,” alisema Fadlu.

## MUKWALA: KIKUBWA POINTI

NA MWANDISHI WETU

NYOTA Steven Mukwala mshambuliaji wa Simba amesema kuwa kazi kubwa ni kupambana kwenye mech zote kupata matokeo mazuri kutokana na ushirikiano ambao upo kwenye timu hiyo inayonolewa na Kocha Fadlu Davids.

Kwenye msimamo wa ligi Simba ni namba mbili baada ya mechi 21 imekusanya jumla ya pointi 54 vinara wakiwa ni Yanga inayonolewa na Kocha Mkuu, Miloud Hamdi.

Simba mchezo wao uliopita wa ligi baada ya dakika 90 ubao ulisoma Coastal Union 0-3 Simba mtupiaji wa mabao yote akiwa ni Mukwala akisepa na tuzo ya mchezaji bora na mpira wake baada ya kufunga hhat trick.

Ni mabao 8 anafikisha Mukwala ndani ya ligi akiwa namba mbili wa wakali wakucheka na nyavu ndani ya kikosi cha Simba ni Jean Ahoua mwenye mabao 10 huyu ni namba moja, Mukwala na Leonal Ateba wote wametupia mabao 8.

Mukwala amesema kuwa kikubwa ambacho wanapambana ni kupata matokeo mazuri na wanaamini kazi itakuwa kubwa kwenye mechi zinazofuata.

“Shukrani kwa mashabiki ambao wapo nasi bega kwa bega kutokana na uwepo wao kwenye mechi zetu zote, ambacho tunapambana ni kupata matokeo mazuri tunaamini itakuwa hivyo kwenye mechi zetu zote.”

Kituo kinachofuata kwa Simba ni Kariakoo Dabi dhidi ya Yanga mchezo unaotarajiwa kuchezwa Uwanja wa Mkapa, Machi 8 2025.



# WAKIZIONA NYAVU LAZIMA ZICHEKENA

MWANDISHI WETU

NDANI ya Ligi Kuu Bara ambayo ni namba nne kwa ubora Afrika kuna wakali wakucheka na nyavu ambao wameandika rekodi zao za kusepa na mipira Bongo msimu wa 2024/25.

Nyota wa kwanza kufunga hat trick ndani ya ligi ni Prince Dube ambaye yupo ndani ya kikosi cha Yanga huyu alifunga kwenye mchezo dhidi ya Mashujaa, Uwanja wa KMC Complex waliposhuhudia ubao ukisoma Yanga 3-2 Mashujaa.

Yanga ni namba moja kwenye eneo la kucheka na nyavu Bongo ambapo safu ya ushambuliaji imetupia mabao 58 na pointi zao kibindoni ni 58 ikiwa inaongoza ligi.

Mkali wa pili kucheka na nyavu akiwa na hat trick ni Aziz Ki ambaye huyu alifunga kwenye mchezo dhidi ya KMC walipoibuka na ushindi wa mabao 6-1 Uwanja wa KMC Complex.

Yanga hat trick zote zimekusanywa Uwanja wa KMC Complex ambapo mchezo mmoja dhidi ya Mashujaa walikuwa nyumbani na mchezo mwingine dhidi ya KMC walikuwa ugenini.

Nyota mwingine ni Steven Mukwala huyu wa Simba alifunga mbele ya Coastal Union, Machi Mosi 2025 Uwanja wa Sheikh Amri Abeid ubao uliposoma Coastal Union 0-3 Simba.

Kituo kinachofuata ni Machi 8, Yanga v Simba, Uwanja wa Mkapa wakali hawa wanatarajiwa kukutana msako wa pointi tatu.

# KOMBE LA SHIRIKISHO WALA HAKUJAPOA

NA MWANDISHI WETU

HUKO Kombe la Shirikisho mnona wanapigika? Wenyeji, JKT Tanzania juzi walifanikiwa kutinga Hatua ya 16 Bora Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), michuano inayodhaminiwa na Benki ya CRDB baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Biashara United ya Mara Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni Jijini Dar es Salaam.

Mabao ya JKT Tanzania yalifungwa na Shiza Kichuya dakika ya 19 na Najim Magulu dakika ya 47, wakati bao pekee la Biashara United lilifungwa na Freddy Kiwale dakika ya 82.

Nayo Tabora United ikaitupa nje Transit Camp kwa penalti 4-2 kufuatia sare ya kufungana bao 1-1 Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Mabingwa wa zamani wa michuano hiyo, Mtibwa Sugar wakaitupa nje Town Stars kwa kuichapa mabao 5-3 Uwanja w Manungu Complex, Morogoro.

Mechi nyingine za Hatua ya 32 Bora, Mbeya Kwanza iliichapa Mambali Ushirikiano mabao 3-0 Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara.

Nao Songea United wakapata ushindi wa 1-0 ugenini dhidi ya Polisi Tanzania Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati Giraffe Academy waliilaz Green Warriors 1-0 Uwanja waUwanja wa Azimio mjini Katavi.

Ikumbukwe Jumapili Azam FC ilitupwa nje ya michuano hiyo baada ya kufungwa na Mbeya City kwa penalti 4-2 kufuatia sare ya 1-1 ndani ya dakika 90 - Mbeya wakianza kupata bao kupitia bao kupitia kwa Daniel William dakika ya 64, kabla ya kiungo Yahya Zaid kuisawazishia Azam FC dakika ya 90’+5.

Kwenye mikwaju ya penalti waliofunga kwa upande Mbeya City ni Adili Buha, Baraka Philemon, David Mwasa na Riffat Msuya, wakati Kilaza Mazoea alikosa – wakati kwa Azam FC ni beki Lusajo Mwaikenda na kiungo Mghana, James Akaminko pekee waliofunga, huku winga Mgambia, Gibril Sillah na beki Nathaniel Chilambo wakikosa.

Mechi nyingine za 32 Bora Jumapili, Singida Black Stars waliitupa nje Leo Tena kwa kuichapa 4-0 Uwanja wa CCM LITI mjini Singida, KMC wakaichapa Cosmopolitan 2-0 Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam na Big Man FC wakaitoa Tanzania Prisons kwa penalti 3-2 baada ya sare ya 1-1 Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

## NYONI AMPA 5 CHAMA

NA MWANDISHI WETU

ERASTO Nyoni kiraka anayetimiza majukumu yake ndani ya kikosi cha Namungo kinachonolewa na Kocha Mkuu, Juma Mgunda ameweka wazi kuwa nyota Clatous Chama amebadilika hasa kwenye upande wa spidi ila watu wanamtazama kwa mazoea.

Ipo wazi kwamba Chama ni mchezaji wa kwanza kutambulishwa ndani ya kikosi cha Yanga kwenye dirisha kubwa la usajili ilikuwa ni Julai Mosi 2024 ambapo aliibuka hapo akiwa ni mchezaji huru baada ya kumaliza kandarasi yake ndani ya kikosi cha Simba.

Chama alipokuwa Simba alikuwa chaguo la kwanza lakini kwa sasa ndani ya kikosi cha Yanga ambacho kwenye anga la kimataifa kimegotea hatua ya makundi sio chaguo la kwanza amekuwa akipokezana namba na Aziz Ki ambaye naye ni kiungo mshambuliaji wakati mwingine Pacome.

Nyoni aliwahi kucheza na Chama katika kikosi cha Simba kabla ya kukutana na Thank You na sasa anaendelea kutimiza majukumu ndani ya Namungo ambayo Februari 27 2025 ilishuhudia ubao wa Uwanja wa Azam Complex ukisoma Azam FC 1-1 Namungo.

Kiungo huyo amesema: “Chama amebadilika kwenye suala zima la uchezaji ila kwa kuwa yupo kwenye timu mpya watu wanamuangalia kwa mazoea tu ninaweza kusema hivyo. Ukimuangalia kwenye uchezaji wake ameongezeka spidi lakini kuna watu hawawezi kujua.

“Ninaweza kusema ni kumzoea si unamuona namna anavyocheza. Watu wamemzoea Chama lakini hawataki kumuona anachezaji kule kuna wachezaji ambao ni wazuri hivyo ushindani utakuwa mkubwa, lakini hapana amebadilika uchezaji mwangalie kwenye mechi zote amebadilika amekuwa kwenye spidi.”


# CHIOMA HANA KITU TUMBONI

LAGOS, Nigeria

MWIGIZAJI wa
ike anayefanya
izuri katika soko
a filamu la Nige-
ia, Chioma Akpo-
ha, amekanusha
aarifa zilizodai
uwa amejifun-
ua.

Ripoti zilizodai
amepata mtoto
a kiume zilivu-
na mitandaoni na
usababisha rafiki
ake, Omoni Obo-
, amtumie ujum-
e wa pongezi.

Hata hivyo, aki-
bu ripoti hizo,
hioma alisema
ntoto pekee ali-
e naye kwa sasa
i chaneli yake
npya ya You-
ube.




# MSIKIE BURNA BOY ANAVYOJIKATAA



LAGOS, Nigeria

STAA wa Afrobeats, Seun Kuti, amejitoa katika bifu linaloendelea kati ya wasanii wawili, Burna Boy na Speed Darlington.

Speed aliwahi kushikiliwa na polisi kwa kosa lake la kumdhalilisha Burna Boy baada ya mwenzake huyo kuhusishwa na P. Diddy.

Sasa, akizungumzia bifu linaloendelea, Kuti alisema: "Nisingependa kuhusishwa na bifu lao. Sisemi kwamba niko upande wa Burna Boy kwa kuwa alinipa dhahabu."

# ARJUN NDO' HIVYO TENA

NEW DELHI, India

STAA wa filamu za Kihindi, Allu Arjun, anashikiliwa na polisi baada ya tukio la watu wawili kupoteza maisha wakiwa 'lokesheni'.

Kwa mujibu wa ripoti, Arjun alikuwa kwenye maandalizi ya filamu yake 'Pushpa 2: The Rule' na aliyepoteza maisha ni mwanamke na mtoto wake wa kiume, huku watu kadhaa wakipata majeraha.

Ripoti zinaeleza kuwa tukio hilo lilisababishwa na maelfu ya mashabiki waliokuwa wamekusanyika nje ya ukumbi uliokuwa unatumika kwa maandalizi.



# ABDALLAH 'KING' KIBADENI

## Fundi wa muda wote Simba SC

NA HENRY PAUL

UNAPOZUNGUMZIA miongoni mwa watu walioiwezesha klabu ya Simba kupata mafanikio makubwa miaka ya nyuma, akiwa mchezaji na kocha wa timu hiyo, kamwe huwezi kuacha kulitaja jina la Abdallah Kibadeni au 'King' kama wapenzi wa soka nchini walivyozoea kumwita.

Wakati wa enzi zake za kucheza soka ya ushindani, Kibadeni ambaye alikuwa anacheza safu ya ushambuliaji wa kati namba 10, alikuwa na kila kitu ambacho mshambuliaji mahiri anatakiwa kuwa navyo ambavyo ni kasi kubwa, chenga za maudhi na uwezo mkubwa wa kupachika mabao.

Nyota huyo ambaye alijiunga na Simba mwaka 1970 akitokea klabu ya Kahe ya Dar es Salaam, mwaka 1973 alikuwa ni miongoni mwa wachezaji walioiwezesha Simba kutwaa Ubingwa wa Soka Tanzania Bara, ambao ulikuwa unashikiliwa na Yanga miaka mitano kuanzia 1968 hadi 1972.

Mbali na mafanikio hayo, pia mwaka huo wa 1973, kibadeni alikuwa katika kikosi kilichoifunga Yanga bao 1-0, lililofungwa na kiungo mshambuliaji Haidari Abeid 'Muchacho' katika dakika ya 68. Mchezo huo wa Ligi Kuu, ulichezwa katika Uwanja wa Taifa jijini (sasa Uhuru), Juni 23, 1973.

Mwaka 1974, Kibadeni alikuwa ni miongoni mwa wachezaji walioiwezesha Simba kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika na kutolewa katika hatua ya mikwaju ya penalti ya mabao 3-0 na Mehara El- Kubra ya Misri.

Katika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo, Simba iliitoa timu ngumu ya Hearts of Oak ya Ghana jumla ya mabao 2-1, yaliyofungwa na Adam Sabu (marehemu) na yeye Kibadeni.

Mchezo wa kwanza ulichezwa mjini Accra, Ghana, huku katika mchezo wa marudiano ulichezwa mjini Dar es Salaam matokeo yalikuwa ni suluhu ya bila kufungana.

Katika hatua ya nusu fainali, Simba ilianza kwa ushindi wa bao 1-0, mjini Dar es Salaam dhidi ya Mehara El Kubra, kabla ya kwenda kufungwa bao 1-0 na Waarabu hao mjini Cairo Misri, hivyo mchezo huo kuhamia katika hatua ya mikwaju ya penalti tano tano na Wekundu hao wa Msimbazi kufungwa mabao hayo 3-0.

Mwaka 1977, Kibadeni akiwa na timu yake hiyo ya Simba, alikuwa ni miongoni mwa wachezaji walioiwezesha kutwaa Ubingwa wa Soka Tanzania Bara na ikiwafunga watani wao wa jadi Yanga mabao 6-0, huku yeye katika mchezo huo akifunga 'hat-trick' mabao matatu, rekodi ambayo haijavunjwa hadi leo hii.



Nyota huyo alifunga mabao hayo matatu katika dakika ya 10, 42 na 89. Mechi hiyo ilichezwa katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Julai 19, 1977. Mabao mengine katika mchezo huo yalifungwa na Jumanne Masmenti dakika ya 60 na 73, huku bao lingine likifungwa na beki wa Yanga Selemani Sanga (marehemu) dakika ya 20 akiwa katika harakati za kuokoa.

Kwa ushindi huo Simba ililipa kisasi cha kufungwa mabao 5-0, iliyofungwa mwaka 1968. Mchezo huo pia ulichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Juni 1.

Mwaka 1990, Kibadeni akiwa kocha, aliiwezesha Simba kutwaa Ubingwa wa Soka Tanzania Bara, huku ikiifunga Yanga katika mchezo wa kwanza bao 1-0, lililofungwa na beki Mavumbi Omari (marehemu) dakika ya sita ya mchezo huo, uliochezwa katika Uwanja wa Taifa jijini Mei 26, 1990.

Mwaka 1991, Kibadeni akiwa kocha mkuu wa timu hiyo ya Simba katika jopo la makocha wanne wasaidizi Omari Mahadhi (marehemu), Salum Madadi na Hassan Affif kama kocha mchezaji, aliiwezesha timu hiyo kutwaa taji la Ubingwa wa Soka Afrika Mashariki na Kati, baada ya kuifunga Club Sports Villa ya Uganda mabao 3-0.

Fainali hiyo ambayo ilikuwa ni kali na ya kusisimua kwa muda wote wa dakika 90, ilichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Februari 16, 1991. Katika mchezo huo Zamoyoni Mogela alifunga mabao mawili na Affif bao moja.

Mwaka 1993, Kibadeni akiwa kocha wa Simba, aliiwezesha timu hiyo kucheza fainali ya michuano ya Shirikisho la Afrika (CAF), na kufungwa mabao 2-0 na Stella Abidjan ya Ivory Coast. Mchezo huo ulichezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Novemba 27, 1993.

Simba ambayo wakati huo ilikuwa na kikosi kizuri, ilitoka suluhu ya bila kufungana katika mchezo wa kwanza, uliochezwa Novemba 14, 1993 mjini Ivory Coast.

Mafanikio mengine ni kwamba mwaka huo wa 1993, akiwa kama kocha aliiwezesha Simba kutwaa Ubingwa wa Soka wa Jamhuri ya Muungano.

Mwaka 1994, Kibadeni akiwa kocha msaidizi chini ya kocha mkuu Mserbia Dragon Popadic, waliiwezesha Simba kutwaa Ubingwa wa Soka Tanzania Bara, huku ikimfunga mtani wake wa jadi Yanga mabao 4-1.

Mwaka 1996, Kibadeni akiwa kocha wa Simba, aliiwezesha timu hiyo kutwaa taji la Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati, baada ya kuifunga APR ya Rwanda bao 1-0, mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini (sasa Uhuru). Bao hilo lilifungwa na mshambuliaji Bita John.

Mei 5, 2012 wakati Simba inaifunga Yanga mabao 5-0, katika mchezo wa marudiano wa Ligi Kuu, Kibadeni alikuwa katika benchi akimshauri kocha mkuu Milovan Cirkovic kutoka Serbia.

Huyo ndiye Abdallah 'King' Kibadeni miongoni mwa watu walioiwezesha Simba kupata mafanikio makubwa akiwa kama mchezaji na kocha.

# YA VERON YAIBUKA KWA ZIRKZEE

ULIMWENGU wa soka umezidi kutuonesha mambo mengi ambayo yanastaajabisha binadamu. Soka limeeendelea kuwa na matukio ya kawaida na yasiyo ya kawaida kama ilivyokuwa zamani.

Moja ya matukio ambayo ni ya kawaida ni kufeli kwa kila makocha na wachezaji katika timu mpya. Lakini pia suala la kushuka au kupanda kwa viwango vya wachezaji ni jambo limezoeleka. Hakuna jambo jepesi kama mchezaji kufanikiwa kufanya vyema katika ligi tofauti au timu tofauti kutokana na utamaduni pamoja na falsafa za maeneo mapya ambayo anakuwa kwa wakati huo.

Manchester United mwanzoni miaka ya 2000 ili msajili kiungo mshambuliaji wa SS Lazio, Juan Sebastian Veron. Ni kiungo mshambuliaji kutoka Argentina ambaye alikuwa na nyakati bora alipokuwa SS Lazio.



Usajili wa Veron ndani ya Manchester united ulifurahiwa na mashabiki wengi. Tangu kuingia hadi kufikia hatua ya kuuzwa Chelsea mchezaji huyo kutoka Argentina hakufikia kiwango alichokionesha pale SS Lazio Jijini Roma nchini Italia.

Hivyo wakati Capello anashangaa yale yanayoendelea kwa Joshua Zirkzee anapaswa kutambua mambo kadhaa kama kocha.

Mazingira yanaweza kumfanya mchezaji akashindwa kufikia malengo. Utamaduni wa Taifa husika unaweza kumfanya mchezaji kushindwa kufikia malengo.

Mchezaji husajiliwa kwa kuzingatia kufikia malengo ya falsafa za klabu. Lakini mchezaji anaweza kufikia malengo ya klabu kama atawezа kuingia haraka katika mfumo wa klabu husika.

Mazingira ambayo yanamkuta Joshua Zirkzee ni kutokana na ugeni wake pamoja na klabu yenyewe kushindwa kufikia matarajio kwa mchezaji.

Mazingira rafiki yanaweza kumfanya mchezaji kufikia malengo ya klabu na kufurahi kazi katika klabu yake.

Kuna kila sababu za benchi la Manchester United kupitia usajili wao na kutazama namna ambavyo wanaweza kuinua kiwango Cha mchezaji.

Joshua ni mchezaji kijana ambaye anaweza kuwa na Kesho nzuri ndani ya klabu na kufikia malengo ya klabu.



# MKUDE

## REKODI YA KIPEKEE KATIKA DABI

NDANI ya Shule ya Msingi Hananasif pale Kinondoni, Dar es Salaam wanamwona kama ni alama yao ya soka. Ni kama ilivyo Shule ya Msingi Barafu pale Mburahati wanavyomwona Salumu Aboubakari 'Sureboy' ni shujaa wao.

Ni kama ilivyo Kwa Mbwana Samatta na Shule ya Msingi Sisimba Jijini Mbeya mitaa ya Jakalanda wanavyomwona kijana wao licha ya kusoma madarasa machache. Hii ni kama ilivyo kwa staa yoyote aliye pata kupita katika taasisi au mitaa yenu na akafanikiwa.

Ni Jonas Gerrard Mkude na Hananasif na Kinondoni yake. Binafsi namwona Mkude kama ilivyo kwa mchezaji aina ya Benoit Assou-Ekotto yule mlinzi wa zamani wa pembeni wa Taifa la Cameroon na Tottenham Hotspur. Lakini pia mchezaji kama Ashley Cole mlinzi wa zamani wa England, Arsenal na Chelsea.

Hawa ni aina ya wachezaji ambao wanacheza soka sababu wanakipaji cha kucheza. Lakini kama utapata kuwafahamu zaidi pengine kama wangekuwa na uwezo wa kufanya mengine basi wangefanya na sio kucheza soka.

Mkude kwake soka ni kazi ambayo anaifanya sababu ya kuwa na kipaji nacho. Hulka na mwenendo wake utakupa tafsiri ya kuwa anacheza soka sababu anakipaji cha soka.

Nimepata kukutana na Mkude mara nne akitembelea ndugu zake walioko Morogoro vijijini, Kijiji cha Kiroka. Hutumia mapumziko Kwa kuwasalimia baba zake wadogo na wakubwa pamoja na shangazi zake.

Akiwa eneo hilo hutomwona hata kufanya mazoezi na timu ya hapo kijijini wala kusogelea hata uwanja wa soka. Anakuwa na mapumziko ambayo yanahitaji kupumzisha mwili baada ya kazi ngumu za msimu mzima.

Wako wachezaji wengi ambao wamepata kuchezea Yanga na Simba katika nyakati tofauti kwa kizazi cha miaka ya hivi karibuni. Hapa nawataja wachezaji kama Athumani Iddi Chuji, Juma Kaseja, George Owino, Mrisho Ngassa, Emmanuel Okwi, Bernard Morrison, Haruna Niyonzima na Hassan Dilunga.



Hata kizazi cha Ivo Mapunda, Shabani Ramadhani, Monja Liseki, Akida Makunda hakuna aliyefikia namba za Mkude .Lakini hakuna mchezaji ambaye anafikia hata nusu ya idadi ya mechi za dabi alizocheza Jonas Mkude.

Jikumbushe kama ule mchezo wa Simba dhidi ya Yanga hapo Oktoba 19 ilikuwa mkakati wa rekodi kwa Jonas Mkude kucheza ule mchezo na alifanikiwa kuingia na kucheza. Hadi Sasa takwimu zinaeleza yeye amecheza mechi 22 za dabi ya Kariakoo. Pengine inawezekana ikawa ni idadi kubwa zaidi kuliko mchezaji yoyote Tanzania kucheza michezo hiyo.

Yawezekana hata watangulizi wake wa kuhama timu moja kwenda nyingine hawakufikiria kuweka rekodi. Yapo majina kama ya Zamoyoni Mogella na Method Mogella, Said Mwamba 'Kizota'. Lakini kufikia rekodi ya Jonas Gerrard Mkude ni jambo lingine ambalo ni gumu kulifikia.

Akiwa Yanga, Mkude amejikuta akiwa nyumbani kutokana na kuwa na wachezaji wenzake wa zamani wa klabu ya Simba yaani Jean Ottos Baleke na Clatous Chota Chama. Awali alikuwa na Agustin Okrah kabla ya Yanga kuamua kuachana nae.

Ni ngumu kuingia katika moyo ya mashabiki wa timu zote mbili. Labda jambo jepesi kwa mchezaji ni kama mchezaji atakuwa ameechwa na sio kushinikiza kutoka katika klabu hiyo.

Kongole kwa 'Living Legend' Jonas Gerrard Mkude naamini maombi na baraka toka kwa familia yake pale Kiroka, Morogoro Vijijini na Kinondoni ni nyingi kwani ni fahari yao uwapo uwanjani

# UTAKAA TU!

## WATAMALIZA MSIMU KWA UBABE ZAIDI

KALENDA ya michezo inapozidi kupamba moto mwaka wa 2025, ulimwengu unatazamiwa kuwa uwanja wa michezo kwa wapenda michezo, huku kukiwa na msururu wa matukio ya kusisimua na burudani za kila aina.

Kuanzia mashindano ya Riadha ya Dunia , michezo ya ndondi na Ligi Kuu za mataifa mbalimbali, kuna burudani kwa kila mtu.

Ifuatayo ni orodha ya wanariadha wa kuwatupia jicho mwaka 2025.

**Lamine Yamal-Hispania**

Mchezaji wa Barcelona na Hispania, Lamine Yamal ameshinda tuzo ya Golden Boy 2024.

Tuzo hiyo iliyoanzishwa na gazeti la Italia la Tuttosport, hutolewa kwa mchezaji bora wa Ulaya kwa wanaume chini ya umri wa miaka 21, huku waandishi wa habari wakipiga kura kwa kutumia mfumo wa pointi.

Yamal, 17, alijiimarisha katika kikosi cha kwanza cha Barcelona msimu uliopita kabla ya kuisaidia Uhispania kushinda Euro 2024.

Winga huyo alifunga bao moja na kusaidia mengine manne huku akitajwa kuwa mchezaji chipukizi bora wa michuano hiyo.

Mnamo Oktoba, Yamal alishinda Kombe la Kopa, zawadi sawa na iliyotolewa wakati wa sherehe ya Ballon d'Or ya 2024.

Yamal amefunga mabao sita na kutoa asisti nane katika mechi 16 za mashindano yote msimu huu.

**Faith Kipyegon-Kenya**

Bingwa wa dunia na Michezo ya Olimpiki, Faith Kipyegon alikuwa na msimu mzuri mwaka 2023 aliposhinda mbio zake zote isipokuwa moja ya mbio zake na kuweka rekodi tatu za ulimwengu.

Kipyegon alivunja rekodi za dunia katika mbio za mita 1,500, 5,000 na maili hiyo kando na kushinda mara mbili dhahabu ya mita 1,500 na 5,000 kwenye Mashindano ya Dunia.

Pia alitwaa Tuzo la Ligi ya Diamond katika mkondo wa mwisho wa msimu, Prefontaine Classic, mafanikio ambayo yalimpa Tuzo ya Mwanariadha Bora wa Kike wa 2023.

Kuelekea 2025, Kipyegon anapendelea zaidi kushinda medali za dhahabu katika mbio za mita 1,500 na kuna matumaini kwamba rekodi zaidi zitaporomoka.

**Noah Lyles-Marekani**

Noah Lyles ni mwanariadha wa Marekani ambaye alijulikana kama 'mtu mwenye kasi zaidi duniani' baada ya kushinda medali tatu za dhahabu-katika mita 100, mita 200, na Relay ya mita 4 × 100-kwenye mashindano ya dunia ya 2023.

Noah Lyles pia alishinda mbio za mita 100 kwa wanaume kwenye Michezo ya Olimpiki ya 2024 , akimshinda Kishane Thompson wa Jamaika kwa . 005 sekunde

**Kylian Mbappe - Ufaransa**

Mchezo wa mshambuliaji wa Real Madrid Kylian Mbappe "uko chini" lakini ana dhamira ya kuvuka kipindi kigumu, kulingana na meneja Carlo Ancelotti.

Fowadi huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25, ambaye alijiunga na Real kwa uhamisho wa bila malipo kutoka Paris St-Germain mwezi Julai, amekuwa na wakati mgumu sana tangu alipowasili Bernabeu.

"Mbappe yuko chini kama kila mtu mwingine, lakini ana ari ya kumaliza kipindi hiki," bosi wa Real Ancelotti aliambia mkutano wa wanahabari.

"Tatizo alilo nalo ni la kila mtu. Unaweza kumwelekeza Vinicius Jr, Rodrygo au Jude Bellingham. Ni wakati mgumu kwa kila mtu."

Mchezaji huyo anatarajiwa kuimarika 2025 wakati ambapo atakuwa amefahamikiana vizuri kimchezo na wachezaji wenzake Real Madrid.

**Beatrice Chebet - Kenya**

Beatrice Chebet ni mwanariadha wa Kenya wa mbio ndefu ambaye ndiye anayeshikilia rekodi ya dunia katika mbio za mita 10,000 na medali ya dhahabu katika michezo ya Olimpiki ya 2024 katika mbio za mita 5000 na 10,000, mbali na kuwa mwanamke wa tatu katika historia kushinda mbio mbili tofauti kwenye michezo ya Olimpiki.

Mwaka 2022, Chebet alishinda medali za dhahabu katika mbio za mita 5000 kwenye Michezo ya Jumuiya ya Madola, Mashindano ya Afrika, na Ligi ya Almasi, na medali ya fedha katika mbio za mita 5000 kwenye Mashindano ya Dunia. Chebet pia alishinda medali za dhahabu katika Mashindano ya Dunia ya 2023 na 2024.

Katika mashindano ya vijana ,Chebet alishinda medali za dhahabu katika mbio za mita 5000 kwenye Mashindano ya Dunia ya U20 ya IAAF 2018 na sehemu ya Wanawake ya Vijana ya Mashindano ya Dunia ya Mbio za Nyika za 2019.

**Gervonta Davis - Marekani**

Gervonta Bryant Davis anayejulikana pia kwa jina lake la utani 'Tank', ni bondia mtaalamu wa Marekani. Ameshikilia taji la Chama cha Ngumi cha Dunia (WBA) uzani mwepesi tangu 2023, akiwa ameshikilia toleo la kawaida kutoka 2019 hadi 2023. Pia alishikilia taji la Shirikisho la Ndondi la Kimataifa (IBF) uzani wa super feather mnamo 2017, taji la WBA super featherweight mara mbili kati ya 2018 na 2020, na taji la WBA super lightweight mwaka 2021.

Kufikia Mei 2024, Davis aliorodheshwa kama mchezaji wa pili bora duniani katika uzani mwepesi na ESPN, kwanza na Bodi ya Nafasi za Ndondi za Kimataifa, na pili na jarida la The Ring.

Amethibitisha kuwa taaluma yake inakaribia mwisho. Akiwa na rekodi nzuri ya mapigano 30 bila kushindwa na 28 ya mtoano, mpiganaji huyo mwenye umri wa miaka 30 ametangaza kuwa ana mpango wa kustaafu mwaka 2025, na kuacha historia ambayo imewashangaza mashabiki na wataalam wengi






Victor Wembanyama - Ufaransa

Nyota wa San Antonio Spurs, Victor Wembanyama ameshinda tuzo ya mchezaji bora anayechipuka wa NBA mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 ndiye Mfaransa wa kwanza kushinda tuzo hiyo baada ya kuwa na wastani wa pointi 21.4

Wembanyama, alipata kura zote 99 za nafasi ya kwanza.

Yeye ndiye Rookie wa kwanza kwa kauli moja tangu Karl-Anthony Towns mnamo 2016.

"Malengo yangu siku zote yalikuwa ni kuisaidia timu yangu kadri niwezavyo na kuwa bora kadri mwaka ulivyosonga," Wembanyama aliambia TNT Sports.

Mchezaji wa timu Oklahoma City Thunder Chet Holmgren aliibuka wa pili na Brandon Miller wa Charlotte Hornets akashikilia nafasi ya tatu.

**Letsile Tebogo - Botswana**

Letsile Tebogo ni mwanariadha kutoka Botswana. Alishinda medali ya dhahabu katika Olimpiki ya 2024 katika mashindano ya mbio za mita 200, na ushindi wake uliipata Botswana dhahabu ya kwanza ya Olimpiki. Pia alishinda medali ya fedha katika Mashindano ya Dunia ya 2023 katika mbio za mita 100 na kufuatiwa na medali ya shaba katika mbio za mita 200 siku tano baadaye.

Tebogo alishinda katika mbio za mita 100 na kushika nafasi ya pili katika mbio za mita 200 katika Mashindano yote mawili ya Riadha ya Dunia ya 2021 na 2022. Mwaka 2021, alikua mwanariadha wa kwanza wa Botswana kushinda taji la mita 100 katika kiwango chochote cha Ubingwa wa Dunia.

Yeye ndiye bingwa wa Afrika wa mita 200 2022 na kuwa mshindi mwenye umri mdogo zaidi wa taji hili katika historia ya mashindano. Alishinda tuzo ya mwanamichezo bora wa dunia upande wa wanaume 2024.

**Amos Serem - Kenya**

Mwanariadha Mkenya Amos Serem alisitisha mfululizo wa ushindi wa miaka 2 wa bingwa mara 2 wa Olimpiki Soufiane El Bakkali na kushinda taji lake la kwanza la Ligi ya Diamond la mbio za mita 3000 kuruka viunzi kwenye Fainali ya Allianz Memorial van Damme – Wanda Diamond League mjini Brussels..

Serem alimzidi El Bakkali kwa urahisi katika awamu ya mwisho na kushinda kwa saa 8:06.90. El bakali wa Morocco alimaliza katika nafasi ya pili kwa muda wa 8:08.60 huku Mohamed Amin Jhinaoui wa Tunisia (8:09.68) akimaliza wa tatu.

Amos Serem ana hamu ya kutwaa tena utawala wa Kenya katika mbio za kuruka viunzi mwaka wa 2025, lengo kuu likiwa ni kung'ara katika Mashindano ya Dunia huko Tokyo, Japan.

**Daniel Dubois - Uingereza**

Daniel Dubois ni mwanamasumbwi mtaalamu wa Uingereza. Ameshikilia taji la uzani mzito la Shirikisho la Ndondi za Kimataifa (IBF) tangu Juni 2024. Hapo awali, aliwahi kushikilia taji la uzito wa juu la Chama cha Ngumi cha Dunia (WBA) kutoka 2022 hadi 2023.

Katika ngazi ya mkoa, amewahi kushikilia ubingwa wa uzani mzito, pamoja na mataji ya Uingereza na Jumuiya ya Madola kutoka 2019 hadi 2020.

Akiwa mwanariadha, alikuwa bingwa mara tano wa kitaifa upande wa vijana na bingwa wa Uingereza. Dubois anajulikana kwa uwezo wake wa ngumi nzito akishinda mara 21 kati ya 22 kwa njia ya knockout.

Ushindi wake mkubwa dhidi ya Bingwa wa zamani wa uzani mzito zaidi duniani Anthony Joshua uliinua nyota yake.

**Faith Cherotich - Kenya**

Faith Cherotich ni mwanariadha wa Kenya ambaye ni mtaalamu wa mbio za mita 3000 kuruka viunzi. Akiwa na umri wa miaka 17, alishinda nishani ya shaba katika Mashindano ya Riadha ya Dunia ya walio chini ya umri wa miaka 20 ya 2021 yaliyoandaliwa Nairobi.

Cherotich aliboresha shaba yake hadi dhahabu mwaka mmoja baadaye, na kushinda taji katika Mashindano ya Dunia ya U20 huko Cali. Mshindi wa medali ya shaba katika Olimpiki, Faith Cherotich alimshangaza bingwa wa Olimpiki na Dunia wa mbio za mita 3,000 kuruka viunzi, Winfred Yavi na kutwaa taji la Diamond League huko Allianz Memorial Van Damme - fainali ya mzunguko wa Diamond League 2024.

# RAMADHANI KILAMBO




UNAPOTAJA wachezaji waliokuwa wanacheza nafasi zaidi ya moja uwanjani waliowahi kuichezea klabu ya Yanga miaka ya nyuma, kamwe huwezi kuacha kulitaja jina la Ramadhani Kilambo ambaye ameichezea klabu hiyo yenye maskani yake makuu Kariakoo misimu miwili 1990/1991 hadi 1991/1992.

Umahiri wa mkongwe huyo ulitokana na aina ya uchezaji wake, kwani wakati wa enzi zake za kucheza soka ya ushindani, alikuwa anacheza kwa umakini mkubwa, huku akijituma katika nafasi yeyote ile, iwe ya ulinzi, kiungo au ya ushambuliaji.

Nyota huyo pamoja na kuanzia kucheza katika timu nyingi ambazo hazikuwa na majina makubwa, lakini alianza kujulikana zaidi msimu wa 1990/1991 alipojiunga na klabu ya Yanga.

Nyota huyo baada ya kujiunga na Yanga miongoni mwa wachezaji aliowakuta na kucheza nao ni Stephen Nemes 'Masajage', Kenneth Mkapa, Godwin Aswile 'Scania', Said Zimbwe (marehemu), Issa Athumani (marehemu), Athumani China, Joseph Machela, Thomas Kipese 'Uncle Thom', Justine Mtekere (marehemu).

Wengine ni Sanifu Lazaro 'Tingisha', Peter Tino, Mohamed Yahaya 'Tostao', Said Sued 'Scud', John Mngazija (marehemu), Willy Mtendamema, Wastara Baribari na Abdallah Selemani 'Kaburu'. Yanga wakati huo ilikuwa ikinolewa na Syllersaid Mziray mbaye hivi sasa ni marehemu.

Mkongwe huyo akiwa na klabu ya Yanga, mechi iliyompandisha chati ilikuwa ni mchezo wa kirafiki wa Kimataifa dhidi ya timu ya Taifa ya Uganda 'The Cranes', uliochezwa katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru) mwaka 1991.

Matokeo ya mchezo huo ambao ulikuwa ni mkali na wa kusisimua kwa muda wote wa dakika 90, yalikuwa ni sare ya bao 1-1. Katika mchezo huo Kilambo alicheza nafasi ya ushambuliaji namba 10, huku akishirikiana vyema na Abdallah 'Kaburu', Sanifu Lazaro 'Tingisha, Wastara Baribari na Abubakar Salum 'Sure Boy'.

Katika mechi hiyo ya kirafiki dhidi ya 'The Cranes', Yanga ilimchezesha beki aliyekuwa Simba wakati huo Deo Njohole 'OCD' akiwa kama mgeni mwalikwa. Njohole aliletwa kucheza katika mechi hiyo ya kirafiki na aliyekuwa mfadhili mkuu wa Yanga wakati huo marehemu Abbas Gulamali.

Msimu wa 1990/1991 wa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara (sasa Ligi Kuu), Yanga dhidi ya Simba, katika michezo yote miwili ambayo Yanga ilishinda bao 1-0 michezo yote, kilambo alikuwa ni miongoni mwa wachezaji wa Yanga waliocheza mechi hizo.

Ikumbukwe kwamba katika michezo yote miwili, bao hilo pekee lilifungwa na mshambuliaji chipukizi wakati huo aliyekuwa anacheza safu ya kati Said Sued 'Scud'.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa katika Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Jumamosi Mei 18, 1991 na 'Scud' alifunga bao hilo pekee katika dakika ya saba na katika mchezo wa marudiano 'Scud' alifunga bao katika dakika ya 59.

Mwaka 1992, Kilambo alihama Yanga na kujiunga na Reli FC ya Morogoro maarufu 'Kiboko cha Vigogo'. Baada ya kujiunga na Reli, nyota huyo akawa ni miongoni mwa wachezaji wa kutegemewa wa klabu hiyo.

Miongoni mwa wachezaji aliowakuta na kucheza nao ni Mwanamtwa Kiwhelo, Boniface Njohole, Juma Salum, Mbui Yondani, David Mihambo na marehemu Duncun Butinini.

Ramadhani Kilambo, pamoja na kuzichezea Yanga na Reli kwa mafanikio, pia amezichezea klabu kadhaa zikiwemo Chuo Sokoine, Canvas zote za Morogoro na timu ya Mkoa wa Morogoro.



# ALIFELI UWANJANI, SASA MKWANJA WA KUTOSHA

KWA miaka mingi, makinda waliotokea katika 'academy' ya Barcelona wamekuwa wakitabiriwa kufikia levo za Lionel Messi. Giovani Dos Santos ni miongoni mwao. Aliwahi kuitabiriwa makubwa akiwa La Masia.

Dos Santos raia wa Mexico, aliwasili Catalunya akiwa na umri wa miaka 12 lakini kiwango chake kikubwa akiwa La Masia alianza kuitumikia Barca ya wakubwa miaka mitano tu baadaye.

Beki wa zamani wa Tottenham, Ledley King, aliwahi kusema: "Nakumbuka niliwahi kumuona Giovanni Dos Santos akiwa na U-16 ya Mexico. Alikuwa kama Ronaldinho mdogo."

Hata hivyo, tofauti na matarajio makubwa waliyokuwa nayo mashabiki wa Barca, Dos Santos alidumu kwa msimu mmoja tu katika kikosi cha wakubwa, kabla ya kuuzwa Tottenham mwaka 2018.

Akiwa Tottenham, bado nyota huyo alishindwa kuwika Ligi Kuu ya England (EPL), ambapo alishia kupelekwa kwa mkopo katika klabu za Ipswich, Galatasaray na Racing Santander.

Baada ya kushindwa kutamba kote huko, Dos Santos alirejea La Liga, safari hii akisajiliwa na Villarreal msimu wa 2013-14, kabla ya kwenda LA Galaxy ya Marekani na kustaafu mwaka 2021 akiwa na Club America.

Sasa, baada ya kufeli huko, Dos Santos mwenye umri wa miaka 35 ni miongoni mwa wanasoka waliofaulu nje ya uwanja.

Ndiyo, anatajwa kuwa na mkwanja mrefu kutokana na biashara ya mafuta ya petroli. Kupitia hisa zake katika Kampuni ya Procura Mexico, winga huyo wa zamani anaingiza hadi Pauni 400,000 kwa mwaka.

Mbali ya biashara hiyo, Dos Santos pia anatajwa kuvuna fedha nyingi kutokana na biashara yake ya uuzaji wa magari, ambayo inafanya vizuri huko kwao, Mexico.



## JOHAN VASQUEZ NINI TENA

LONDON, England

TIMU za Brentford na Fulham zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili beki wa Mexico Johan Vasquez, 26, kutoka Genoa.

Fulham na Sporting wanamuwinda beki wa Ugiriki, Georgios Vagiannidis, huku Sporting wakiwasilisha dau la euro 10m (£8.3m) kwa Panathinaikos.




# MADRID YAMSAKA WHARTON




MADRID, Hispania

WASAKA vipaji wa Real Madrid wamekuwa wakimfuatilia kiungo wa England Adam Wharton tangu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 arejee kwenye kikosi cha kwanza cha klabu ya Crystal Palace.


Nayo Liverpool wameanza mazungumzo na Conor Bradley kuhusu kandarasi mpya ya miaka mitano ambayo itamuwezesha beki huyo wa Ireland Kaskazini, 21, kupata nyongeza ya 650%.

# TAH KUTOKA LEVERKUSEN

LEVERKUSE, Ujerumani

BEKI wa Ujerumani Jonathan Tah, 29, ataondoka Bayer Leverkusen kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu.

Gwiji wa zamani wa a Atletico Madrid Andrea Berta anaaminika kuwa miongoni mwa watu wanaotarajiwa kuchukua nafasi ya Edu kama mkurugenzi wa michezo wa Arsenal.








# BADO SIJAMKATIA TAMAA MANULA

KIKOSI cha Simba kina jumla ya walinda mlango watano. Pengine hii nayo ni rekodi ambayo imeandikwa kwa klabu Kuwa na makipa wengi kwa wakati mmoja.

Aishi Manula, Ally Salim, Hussein Abel, Ayoub Lakred na Moussa Camara. Ni idadi kubwa ya wachezaji wa nafasi moja uwanjani. Wakati haya yakizidi kuifanya Simba kuwa klabu ya tofauti, unaona imani ya mashabiki na Watanzania juu ya makipa wao.

Katika orodha ya makipa hao. Manula anakuwa ndiye kipa mwenye uzoefu mkubwa sana katika soka la Tanzania na nje ya mipaka ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa. Nyakati zote ambazo Simba aliweza kuingia hatua ya robo fainali michuano ya Caf, lango lililkuwa chini ya Manula.

Hivyo, licha ya changamoto ambazo amekutana nazo katika soka, lakini imani yangu lwa Manula ni mtu sahihi sana awapo langoni. Kwa sasa unaweza kusema amepoteza mvuto mbele ya mashabiki ila kazi ambayo imefanywa na uongozi wa TFF ni ya kupongezwa sana.

Baada ya kuona uhitaji wa Manula ni mkubwa walianza kumjumuisha katika timu ya wachezaji wa ndani. Yaani alikuwa mahodha wa CHAN Kwa timu ya taifa.

Kikosi chetu kikiwa na idadi kubwa ya wachezaji ambao wanacheza klabu za kati ambavyo sio Simba na Yanga. Kazi ambayo ameifanya Manula katika mechi mbili dhidi ya Sudan nyumbani na ugenini imetoa picha halisi uwezo wake na alivyo.

Changamoto ya kukatiwa tamaa na viongozi pamoja na baadhi ya mashabiki hali hiyo ilianza katika mechi ya Simba na Yanga baada ya kupoteza kwa idadi kubwa ya magoli yaani 1-5. Lakini ni jambo ambalo kilachezaji anaweza kukutana nalo.

Arsenal ilipata kupoteza kwa idadi kubwa bao 8-2 dhidi ya Manchester United. Wakati huo pia Manchester United ilipata kupoteza kwa idadi kuwa ya mabao 1-6 katika Uwanja wa Old Trafford dhidi ya Manchester City.

Lakini pia kupoteza kwa idadi ya magoli 7-1, 6-0 kwa klabu kama vya Liverpool na Tottenham Hotspur. Vichapo vyote vilitokea wakati David De Gea akiwa langoni na bado aliendelea kuwa kipa namba moja wa klabu hiyo.

Kurejea kwa Manula katika timu ya taifa yaani Taifa Stars kumefanya aanze na 'Clean sheet' dhidi ya Ethiopia. Naweza kusema Manula ndiye Guillermo Ochoa wetu kwa Tanzania.

Makipa walio wengi katika klabu tofauti nchini hasa Watanzania. Wamekuwa wakimwona Manula kama ndiye 'role model' wao. Maisha ya kisoka. Namna anavyo cheza, namna anavyoongea katika mahojiano lakini pia uvaaji wake ndani na nje ya uwanja wengi humtazama Manula.

Tulimhitaji Manula na bado tunamhitaji Manula katika soka la Tanzania. Binafsi imani yangu inakuwa kubwa sana ninapo ona lango la Tanzania au Simba linalindwa na Manula.

Kitu pekee anaweza kukifanya ni kurejesha ubabe wake langoni machoni pa watu. Bado sijamkatia tamaa Manula na naamini ataendelea kuishi katika milingoti mitatu ya uwanjani.

# JAY Z ALIJIFICHA KISA TUPAC


LOS ANGELES, Marekani

KWA mujibu wa mlinzi binafsi wa zamani wa P. Diddy, Jay Z aliwahi kujificha chumbani akihofia kudundwa na Tupac.

Mlinzi huyo, Gene Deal, alisema kama si Suge Knight aliyekuwa bosi wa Tupac kuingilia kati, basi Jay Z asingetoka chumbani siku hiyo.

Gene Deal aliongeza kuwa siku hiyo Jay Z alikuwa na shoo mjini Las Vegas lakini alishindwa kutoka hotelini baada ya kusikia kuwa 'adui' yake, Tupac, alikuwa nje akisubiri wazipige.





# LAMAR ATAJA RAPA BORA

LOS ANGELES, Marekani

STAA wa muziki wa Hip hop, Kendrick Lamar, ametoa maoni yake juu ya rapa bora zaidi kwa mwaka wa 2024.

Labda wengi wangedhani Lamar angewataja Nicki Minaj na marapa wengine wenye majina makubwa.

Na badala yake, Lamar alisema bibiye Doechii ndiye rapa wake wa kiwango cha juu kwa mwaka huu.

# KANYE AJIBU SHUTUMA ZAKE

LOS ANGELES, Marekani

RAPA asiyeishiwa na matukio, Kanye West, ameyaita kuwa ni uzushi madai ya mfanyakazi wake wa zamani, Lauren Pisciotta.

Pisciotta aliibuka hivi karibuni akidai kuwa Kanye aliwahi kumfanyia udhalilishaji wakati wakiwa pamoja kwenye kazi.

Kwa mujibu wa bibiye huyo, Kanye alikuwa akimlazimisha kufanya mapenzi wakati wakiwa kwenye maandalizi ya albamu yake ya 'Donda' mwaka 2021.



# DONDOO

## HUYU GUARDIOLA MUACHE TU

MANCHESTER, England

KOCHA wa Manchester City Pep Guardiola anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Uingereza Jack Grealish, 29, huku kukiwa na mipango ya kukimarisha kikosi cha City.

Inter Milan wanaibuka wapinzani wakuu wa Liverpool katika mbio za kumsajili kiungo wa Ujerumani Joshua Kimmich huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 akiingia akisalia na miezi michache katika mkataba wake na Bayern Munich.

## PEDRO AJIPIGIA DEBE

LONDON, England

MSHAMBULIAJI wa Brighton wa Brazil Joao Pedro, 23, anataka kujiunga na Liverpool majira ya joto.

Naye straika wa wa Canada Jonathan Davidyuko tayari kuondoka katika klabu hiyo kama mchezaji huru msimu huu wa joto.

## BART MBIONI KUTWALIWA

LONDON, England

CHELSEA inamfuatilia kwa karibu kipa wa Uholanzi na klabu ya Brighton Bart Verbruggen, 22, kwa ajili ya uhamisho wa majira ya joto.

Nazo Manchester United, Tottenham na Arsenal zimeonyesha nia ya kumsajili Benjamin Sesko kutoka RB Leipzig na mshambuliaji huyo wa Slovenia mwenye umri wa miaka 21 ana kipengele cha kutolewa ambacho kinaweza kutumika msimu huu wa joto.


# NICK POPE KUUZWA TU

LONDON, England

NEWCASTLE ikotayari kumuuza mlinda lango wao wa Uingereza Nick Pope, 32, kwa kati ya pauni milioni 10-15 na wana nia ya kumbadilisha na kipa wa Burnley mwenye umri wa miaka 22 James Trafford.

Barcelona inatazamia kuongeza mkataba wa winga wa Brazil Raphinha, 28.

Nayo Chelsea bado iko mbioni kumsaka kiungo wa Gremio na Brazil Gabriel Mec, 16.



JUMATANO MACHI 5 , 2025
SPORT MASTA




# WAMEPIGWA!

## MKONGWE APONDA MADRID KUMSAJILI KYLIAN MBAPPE

LILLE, Ufaransa

MKONGWE wa Ligue 1, Ludovic Obraniak, ameuponda usajili wa Kylian Mbappe akisema Real Madrid walisajili ukubwa wa jina la mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Obraniak aliyewahi kutamba Ligue 1 akiwa na Lille, si mkongwe pekee aliyekosoa usajili huo. Hivi karibuni, lejendari wa Ligi Kuu ya England (EPL), Troy Deeney, naye alitoa maoni ya aina hiyo.

Mbappe aliondoka PSG majira ya kiangazi na kutua Santiago Bernabeu lakini makali yake ya kuzipasia nyavu yamepotea tangu alipohamia Ligi Kuu ya Hispania (La Liga).

Tangu aliposajiliwa, Mbappe amekosa mwendelezo wa kiwango bora, licha ya kufunga mabao nane na kutoa pasi za mabao (asisti) mbili katika mechi zake 16 alizoshuka dimbani akiwa na Madrid.

Akihojiwa na mtandao wa So Foot, Obraniak alisema ingekuwa bora zaidi endapo nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 angeamua kubaki jijini Paris.

“Ilikuwa mapema. Nafikiri alipaswa kubaki kama alivyofanya mwaka 2022. Madrid nao ni kama waliharakisha,” alisema Obraniak.

Kwa upande wake, Deeney alisema hatua ya Madrid kumsajili Mbappe illenga zaidi kujinufaisha katika biashara ya mauzo ya jezi.

“Ni usajili ambao wengi wetu hatukuutarajia. Kwa upande wangu, ni tofauti na Manchester City walipomsajili (Erling) Haaland,” alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa Burnley.

Katika hatua nyingine, Deeney alisema usajili wa Mbappe haukuwa na tija kwa kuwa Mfaransa huyo siyo straika halisi. “Pia, hawezi kucheza winga ya kushoto kwa kuwa tayari kikosi kina Vinicius Jr.

“Ukiniuliza, nitakwambia Madrid walifanya kosa kubwa. Walisajili mchezaji wa kuuzia jezi na kuifanya klabu iwe maarufu zaidi, si mchezaji wa kuisaidia timu kupata matokeo,” alisisitiza Deeney.




## MAN U YAJIPANGA KWA OSIMHEN

MANCHESTER, England

TIMU ya Manchester United inataka kumsajili mshambuliaji wa Nigeria Victor Osimhen, 26, kutoka Napoli, ambayo inatathmini uwezekano wa kumpata mshambuliaji wa Denmark Rasmus Hojlund, 22, kama sehemu ya huo.

Wakati huo huo, Manchester United ina mpango wa kumnunua kiungo wa Real Sociedad na Uhispania Martin Zubimendi, 26.

Nazo Manchester City na Manchester United zinamfuatilia kwa karibu winga wa Ureno Francisco Trincao, ingawa Sporting ina matumaini ya kufikia kandarasi mpya na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

Everton inataka kumsajili winga wa Brazil Luis Henrique, 23, kutoka Marseille msimu huu wa joto lakini watakabiliana na ushindani kutoka kwa Newcastle na Nottingham Forest.

Liverpool inamfuatilia beki wa Denmark Anton Gaaei, 22, na mshambuliaji wa Ubelgiji Mika Godts, 19.

Tottenham iko tayari kuongeza dau lao ka pauni milioni 8.5 kumsajili mshambuliaji wa Ujerumani Timo Werner msimu huu wa joto baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuondoka RB Leipzig kwa mkopo.